**THE NELSON MANDELA**
**AFRICAN INSTITUTION OF SCIENCE AND TECHNOLOGY**
**(NM-AIST)**

**Office of the Vice Chancellor**

Direct Line: +255 272970001
Mobile Phone: +255 784777580
Fax: +255 272970016
E-mail: vc@nm-aist.ac.tz

**Tengeru**
**P.O. Box 447**
**23311 Arusha**
**TANZANIA**
Website: www.nm-aist.ac.tz

**TANGAZO LA NAFASI YA KAZI KWA FUNDI MKUU WA UJENZI (LOCAL FUNDI IN BUILDING WORKS)**

**UJENZI WA JENGO LA BWENI LA GHOROFA (MULTISTOREY BUILDING):**

***Tarehe : 29/09/2021***

***RE - ADVERTISED***

Kwa kusudi la kuboresha mazingira ya kufundishia na kuongeza udahili, **Taasisi ya Afrika ya Sayansi na Teknolojia ya Nelson Mandela**, inatarajia kujenga jengo la bweni (Hostel) ya ghorofa tatu (Multistorey Building) ndani ya eneo la Taasisi.

Mradi huu unatekelezwa kwa utaratibu wa'FORCE ACCOUNT'kama ilivyoelekezwa na Serikali kupitia miongozo mbalimbali na kusimamiwa na kitengo cha kusimamia miradi cha Chuo cha Ufundi Arusha (ATC-Production and Consulting Bureau).

Hivyo Makamu Mkuu wa Chuo kwa kupitia kamati ya mradi wa Ujenzi anawatangazia wananchi wote wenye uwezo, sifa na uzoefu wa kufanya kazi tajwa hapo juu katika fani, sifa na masharti kama yaliyoainishwa katika tangazo hili kuomba kazi katika fani zifuatazo:

**A) FANI NA MASHARTI/SIFA MAHUSUSI ZA MAFUNDI MKUU ZINAZOHITAJIKA;**

**SIFA ZA FUNDI MKUU UJENZI (UASHI, KUPAUA, RANGI, UMEME NA BOMBA):**

1) Kwa kuzingatia ukubwa wa kazi hii Fundi mkuu lazima awe Mhandisi wa ujenzi (Civil and or related Civil Engineering), Fundi Sanifu Ujenzi (FTC/Diploma) Msanifu majengo (Architect) au Mkadiriaji majenzi (Quantity Surveyor) mwenye uzoefu wa miaka angalau mitano. Fundi mkuu Lazima aambatanishe cheti cha shahada au FTC/Diploma, mikataba ya kazi alizowahi kufanya pamoja na 'CV'yake.

2) Fundi mkuu lazima awe na mafundi wasaidizi angalau watatu (03) kwa kila fani tajwa hapo juu (Uashi, Kupaua, Rangi, Umeme na Bomba).

3) Gharama za kukodi mitambo na vifaa vya kufanyia kazi hii zitagharamiwa na Taasisi ya Afrika ya Sayansi na Teknolojia ya Nelson Mandela.

4) Kwa kuwa hakutakuwa na malipo ya awali kwa fundi mkuu na kwa kuzingatia ukubwa wa kazi hii (Jengo la ghorofa ), lazima fundi mkuu awe na mtaji ili amudu kuwalipa mafundi wake wasaidizi na

awasilishe pamoja na nyaraka zake nakala ya taarifa ya benki (bank statement) ya mwezi wa tisa (Septemba 2021), ili kuthibitisha mtaji alionao wa kuwalipa mafundi wake wasaidizi na vibarua watakao fanya kazi hii.

5) Awe amewahi kufanya kazi inayofanana na hii na **LAZIMA** aambatanishe nyaraka zifuatazo ili kuthibitisha kuwa ni kweli amewahi kufanya na kukamilisha bila shaka:
   a) Mkataba wa kazi inayofanana na hii
   b) Barua ya kupendekezwa (recommendation letter) kutoka kwa Mwajiri wa awali kwa kazi hiyo.

6) Awe na uwezo wa kusoma michoro na kufanya makadirio ya mahitaji (materials).

7) Mafundi wake lazima wawe na uwezo wa kujenga kwa tofali aina zote.

8) Mafundi wake lazima wawe na uwezo wa kupaua paa za aina mbalimbali katika majengo ya serikali.

9) Mafundi wake lazima wawe na uwezo wa kupaua mabati ya aina zote na kufanya '*brandering & ceiling*'.

10) Mafundi wake lazima wawe na uwezo wa kuweka sakafu za aina mbalimbali (za kawaida,tiles,terrazo n.k).

11) Mafundi wake lazima wawe na uwezo wa kutumia mitambo na vifaa mbalimbali vya ujenzi.

12) Mafundi wake lazima wawe na uwezo wa kufanya kazi za usukaji umeme na bomba (Plumbing)

13) Fundi lazima aandae na kuwasilisha mpango kazi ukielezea shughuli na muda wa utekelezaji wa mradi sambamba na nyaraka nyingine katika tangazo hili.

14) Fundi mkuu lazima awasilishe bahasha moja ambayo itakuwa na nyaraka tajwa katika tangazo hili ikiwa pamoja na gharama za ufundi.

15) Nakala ya Michoro na fomu za mchanganuo wa shughuli za ujenzi za mradi huu zinapatikana katika Ofisi ya Ununuzi na Ugavi ya Taasisi Afrika ya Sayansi na Teknolojia ya Nelson Mandela.

16) Mwombaji anatakiwa kudurufu (photocopy) nakala ya michoro na mchanganuo wa shughuli za ujenzi (Schedule of Labour) kwa **gharama zake mwenyewe** ili kujaza na kuwasilisha.

17) Fundi **lazima** aombe na kujaza kazi zote (Uashi, Kupaua, Rangi, Umeme na Bomba) kama ilivyooneshwa katika tangazo hili. Fundi ambaye ataacha kujaza kipengele kimojawapo miongoni mwa vipengele tajwa hapo juu maombi yake hayatafanyiwa kazi.

**18)** Inasisitizwa kuwa fundi mkuu anatakiwa kujaza **gharama za ufundi tu (Labour Charges)** kwa kazi tajwa na kusudiwa kwa mujibu wa tangazo hili.

**B) MASHARTI YA JUMLA KWA MWOMBAJI;**

1) Mwombaji **LAZIMA** awe raia wa Tanzania mwenye umri wa kuanzia miaka 18.
2) Mwombaji **LAZIMA** awe na Namba ya Utambulisho ya mlipa kodi (TIN).
3) Mwombaji **LAZIMA** awe na Akaunti ya benki iliyo hai.

4) Mwombaji **LAZIMA** aandike barua ya maombi kwa jina lake na siyo kampuni au jina la biashara.
5) Maombi yatakayowasilishwa kwa njia ya 'ki-eletroniki'na posta hayatapokelewa.
6) Mwombaji **LAZIMA** aambatanishe barua ya utambulisho kutoka Ofisi ya Serikali ya Kijiji/Mtaa anapoishi.
7) Mwombaji L**AZIMA** awe tayari kufanya kazi muda wa usiku na siku za mwisho wa wiki itakapolazimika kufanya hivyo.

8) Barua za maombi ziwasilishwe kwa njia ya mkono katika ofisi ya Ununuzi na Ugavi ya Taasisi Taasisi ya Afrika ya Sayansi na Teknolojia ya Nelson Mandela ( NM-AIST) zikiwa zimeandikwa juu ya bahasha kwa herufi kubwa:

**MWENYEKITI,**

**KAMATI YA UJENZI,**

**MRADI WA UJENZI WA JENGO LA BWENI (MULTISTOREY BUILDING),**

**S.L.P 447 ARUSHA.**

9) Mwisho wa kupokea Maombi ni tarehe **7/10/2021 saa (nne kamili) 04:00 asubuhi** na ndiyo siku ya ufunguzi wa bahasha za maombi ya mafundi kwa kazi hii.

10) Kwa maelezo fika ofisi za Ununuzi na Ugavi Wing A, Floor ya chini, Chumba Na. A110, Old Moshi/Barabara ya Nelson Mandela, S.L.P 447, Arusha kuanzia saa (tatu kamili) 09:00 asubuhi mpaka saa (tisa na nusu) 3:30 mchana, kwa siku za kazi tu.

11) Siku ya kutembelea na kuona eneo la ujenzi ni **tarehe 04/10/2021 saa (nne kamili)04:00 asubuhi**

## Tangazo hili Limetolewa na:

**Makamu Mkuu Wa Chuo**
**Taasisi ya Afrika ya Sayansi na Teknolojia ya Nelson Mandela ( NM-AIST)**
**S.L.P 447 Arusha.**